

# Bima ya Afya

## Wakati Huna Medicaid



**Huduma ya afya nchini Marekani ni ghali. Kukaa hospitalini kwa siku tatu kunag-harimu karibu \$30,000. Unahitaji bima ya afya ili kujilinda iwapo utaugua au kuumia.**

Bima pia hulipa ziara ya kila mwaka kwa daktari wako. Hii inaweza kusaidia kuzuia matatizo makubwa ya afya katika siku zijazo.

Wakimbizi wanapata Medicaid kwa miezi 12 ya kwanza nchini Marekani. Medicaid ni mpango wa serikali unaolipia huduma yako ya afya. Ni bila malipo kwa wanachama wake na ina faida nzuri sana. Katika Colorado, Medicaid inaitwa Health First Colorado.

Baada ya miezi 12, huenda usiruhusiwe kukaa kwenye Medicaid ikiwa mapato yako ni makubwa sana. **Ukipoteza Medicaid yako, usikae bila bima ya afya! Una siku 60 za kupata bima mpya.**

Una chaguzi kuu mbili: bima kupitia kazi yako, au bima unayonunua kivyako.

### Vikomo vya Mapato kwa Medicaid

*Kikomo cha mapato ili kuhitimu Colorado Medicaid hutofautiana kulingana na ukubwa wa kaya yako na mapato yako.*

**Ukubwa wa familia (vikomo vya 2024):**

<b>Mtu 1:</b>	Hadi \$1,669 kwa mwezi
<b>Watu 2:</b>	Hadi \$2,265 kwa mwezi
<b>Watu 3:</b>	Hadi \$2,862 kwa mwezi
<b>Watu 4:</b>	Hadi \$3,458 kwa mwezi
<b>Watu 5:</b>	Hadi \$4,054 kwa mwezi
<b>Watu 6:</b>	Hadi \$4,651 kwa mwezi

**Wanawake Wajawazito:**  
Hadi \$2,447 kwa mwezi

## Chaguzi Mbili Kuu kwa Bima ya Afya

### 1 Bima Kupitia Kazi Yako

*Hii ndiyo chaguo bora kwa watu wengi. Wamarekani wengi wazima wana bima kupitia kazi zao.*

#### Jinsi ya kujisajili:

Zungumza na mwajiri wako kuhusu kupata bima. Ulizia mtu wa rasilimali watu.

Ikiwa mwajiri wako anasema lazima usubiri hadi mwisho wa mwaka, waambie umepoteza Medicaid, ambayo inakuwezesha kujisajili kwa bima kupitia kazi yako mara moja.

Tovuti hii ya serikali inaonyesha kuwa una siku 60 za kujisajili na mwajiri wako baada ya Medicaid yako kuisha: <https://www.healthcare.gov/coverage-outside-open-enrollment/special-enrollment-period/>

### 2 Bima Unayonunua Kivyako

*Baadhi ya kazi hazitoi bima ya afya. Ikiwa kazi yako haitoi bima, bado unaweza kununua bima peke yako kupitia Connect for Health Colorado.*

Hii inaweza kuwa ghali zaidi kuliko bima kupitia kazi yako. Lakini isipokuwa upate pesa nyingi, utapata usaidizi wa serikali ili kupunguza bili yako ya kila mwezi.

#### Jinsi ya kujisajili:

Vikundi vingi vina watu ambao wanaweza kkusaidia kujisajili kwa bima. Tafuta moja ilioy karibu nawe kwenye tovuti hii:

<https://connectforhealthco.com/we-can-help-assisters/> au piga simu kwa 855.752.6749.

# Kuelewa Gharama za Bima ya Kibinafsi

Bima ya kibinafsi ina aina tatu za malipo.



## 1. Malipo ya kila mwezi.

Hii ndio bei unayoona wakati wa kujisajili kwa mpango wa bima. Malipo yanaweza kugharimu dola mia kadhaa kwa mwezi kwa familia.



## 2. Malipo ya pamoja.

Unapomwona daktari au kupata dawa, unaweza kutozwa malipo ya pamoja. Kiasi kinatofautiana kulingana na huduma. Inaweza kuwa \$5 kwa dawa au \$1,000 kwa kukaa hospitalini.



## 3. Bima ya pamoja.

Mpango wako wa bima utagharamia sehemu kubwa ya gharama ya huduma, lakini bado utalazimika kulipa kati ya 10% hadi 40%, kulingana na aina ya mpango wa bima ulio nao. Ikiwa mpango wako wa bima una malipo ya chini, utahitaji kulipa zaidi kwa bima ya pamoja.

## Viwango vya Chuma

Kadiri malipo yalivyo ghali zaidi, ndivyo faida inavyokuwa bora zaidi. Kwa bei nafuu, zaidi utalipa kwa daktari au hospitali.



### Mipango ya bima ya kiwango cha shaba

ni ya watu wenye afya nzuri ambao wanadhani hawatahitaji huduma nyingi za afya. Lakini unaweza kuishia kulipa pesa nyingi ikiwa utaumia katika ajali.



### Mipango ya bima ya kiwango cha dhahabu

ni ya watu wanaojua watakuwa na gharama kubwa za huduma za afya. Utalipa zaidi katika malipo yako ya kila mwezi, lakini kidogo kwa daktari au hospitali.



Imetayarishwa na: